# MWONGOZO

# KARATASI YA TATU

## SEHEMU A

## 1. HADITHI FUPI (SWALI LA LAZIMA)

**a. Dondoo ( Toba ya Kalia)**

i. Haya ni maneno ya mwandishi akimrejelea Bi Gathoni akiwa kwenye Runinga ya Kikwetu katika kipindi cha nyumbani ni nyumbani.Siri alikuwa anasimulia namna alivyopata ufadhili wake wa Kusomea Uandishi China.

**ii. Umuhimu wa mhusika mrejelewa**

1. Anaendeleza ploti.
2. Anaibua sifa za wahusika wengine
3. Anawatambua wahusika kama vile Jack,na siri
4. Anaendeleza mtindo kama vile mbinu rejeshi
5. Anaendeleza dhamira ya hadithi
6. Anaendeleza anwani
7. Anaendeleza maudhui kama vile teknolojia

**PUPA**

**b. Jinsi Majazi yametumika kujenga vipengele vifuatavyo;**

**i. Wahusika**

- ✓ Mwakuona

Binti huyu ameona mengi katika maisha. Anazaliwa katika familia ya kimaskini na kukabiliwa changamoto chungu nzima

- ✓ Bi. Mtego

Mbinu inayotumika kunasa. Anawekea Mwakuona mtego na kumnasa kisha anamtumbukiza kwenye uzinzi.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

- ✓ Mwinamo

Ina maana ya kupinda kwenda mbele. Ni mtaa duni ambao una vyumba vibovu.

- ✓ Mashaka

Maana ya shida anazopitia mtu maishani. Msichana huyu anapitia mengi chenga ways baada ya kutoroshwa.

- ✓ Bwana na Bi. Mtondo

Siku baada ya kesho kutwa. Hawana matumaini ya kuimarika. Wanajushughulisha kupata lishe ya siku, ya mtondo haiwahusu

- ✓ Chenga –ways

Maanake ni nia zisizo wazi. Mashaka anatamani kutoroka Lakini njia za kufanya hivyo zinaishia kuwa chenga sana kwake.

- ✓ Bwana mpevu

Mwalimu wa Mwakuona. Ana mawazo mapevu kulingana na ushauri anaowapa.

**ii. Maudhui**

- ✓ Yanaendeleza maudhui ya umaskini – Mwakuona anazaliwa katika familia ya kimaskini na kukabiliwa na matatizo chungu nzima.
- ✓ Yanaendeleza maudhui ya elimu – Mwalimu Bwana Mpevu anawapa ushauri unaowafanya wawe wapevu ili wafanye maamuzi ya busara.
- ✓ Yanaendeleza maudhui ya uzinzi – Bi. Mtego anamtega na kumwingiza Mwakuona kwenye danguro.
- ✓ Yanaendeleza maudhui ya ufisadi – Mwakuona analaumu serikali kwa kufumbia macho biashara haramu inayoendelezwa huko Chenga – ways.
- ✓ Yanaendeleza maudhui ya ulaghai – Bi. Mtego anamhandaa kwa ahadi ya kumpeleka Mwakuona ng'ambo na kuyaboresha maisha yake kisha anampeleka kwenye danguro.


Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

# SEHEMU B ( NGUU ZA JADI )

**2a.** Msemaji ni Sagilu, akimwambia Mtemi Lesulia. Yalikuwa mazungumzo ya simu. Hii ni baada ya Lesulia kupata habari Lonare amepatikana na wafuasi wake walikuwa wamemiminika vituoni kupiga kura.

b. Toni ya kuliwaza

Sagilu anambembeleza Lesulia kwamba asiwe na pupa Kwani ni mapema kujua atakayeshida.

c. **Sifa za Msemaji (Sagilu)**

- ✓ Ni mzinzi
- ✓ Ni katili
- ✓ Ni mnafiki
- ✓ Ni mwenye ukiritimba
- ✓ Mwenye kivuli/ dharau
- ✓ Ni msaliti
- ✓ Ni mpenda anasa
- ✓ Mwenye chuki

**d. Athari za ulevi katika nguu za jadi**

- ✓ Kupoteza kazi- Mrima alipigwa kalamu
- ✓ Kuacha shule- Rafiki za Ngoswe walikataa shule baada ya kuingilia mihadarati
- ✓ Kupotoka kimaadili- Wasichana waliomezwa kwenye ukahaba
- ✓ Magonjwa – Mrima alipelekwa hospitalini kutibiwa akili.
- ✓ Kutozingatia usafi – Baada ya Mrima kuingilia ulevi alikuwa mchafu
- ✓ Utekelezaji wa familia – Mrima anamwachia mangwasha majukumu ya kifamilia.

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

3 a. **Mbinu za Kimtindo**

- ✓ Mbinu rejeshi – Waketwa walikuwa na maarifa tangu zamani.
- ✓ Uradidi wa silabi- Silabi ‘ki’ mfano Kichaka kikavu kilichohama
- ✓ Tabaini – Si majumba makubwa ya aushi, Si ghorofa na wingi wa maduka
- ✓ Taswira oni – Nyumba zilizojengwa kando ya biashara
- ✓ Tashbihi- …kama wahamaji…

B . **Dhuluma dhidi ya wanamme ukirejelea Nguu za Jadi**

- ✓ Lonare kutekwa nyara na akina Sagilu
- ✓ Sagilu kutembea na Cheiya Mpenziwe Mashauri mwanawe
- ✓ Sagilu kutorokwa na bibiye baada ya kuwa kichaa.
- ✓ Mrima kupewa pesa na Sagilu na kuingilia ulevi.
- ✓ Cheiya anamdhulumu Mashauri kwa kukubali kufanya usuhuba na babake.
- ✓ Nanzia anamdhulumu Mtemi Lesuilia kwa kufanya usuhuba na Sagilu na yule Mhindi.
- ✓ Mbwashu anamdhulumu Mtemi Lesulia kwa kutorokea ulaya baada ya yeye kushindwa uchaguzi mkuu
- ✓ Sagilu alimdhulumu Mtemi Lesulia kwa kumhakikishia kuwa kila kitu kiko sawa iwapo alijua hangeshida ule ucahguzi mkuu.
- ✓ Mtemi Lesulia alimdhulumu Mwanasheria Mafamba kwa kumnyang’anya cheti cha uanasheria licha ya yeye kufanyia serikali yake kazi na kumfichia uovu wake katika kesi.
- ✓ Mashauri kutoroka chama cha akina babake Sagilu baada ya yeye kuzinzi na mpenziwe.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

# SEHEMU C ( BEMBEA YA MAISHA)

# Dondoo

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

4a. Msemaji ni Luka akiwaambia Beni na Yona wakiwa nyumbani kwa Luka. Hapa alikuwa anaeleza jinsi mtoto wa kike ana thamana kama yule wa kiume ikilinganishwa na zamani ambapo walikuwa wanaamini kuwa mtoto wa kike ataolewa akuache.

b. Toni ya Furaha

Luka anafurahia kuwa kijiji kina mwanga

C . Istiara- walikuwa nyota ya jaha

Mbinu rejeshi – Walikuwa nyota ya Jaha

Jazanda – Nyota ya Jaha

D **. Umuhimu wa mzungumzaji (Luka)**

- ✓ Anaendeleza maudhui ya mabadiliko
- ✓ Anawaunganisha wazee
- ✓ Ameshikilia utamaduni- Kusherehekea mavuno ya kwanza.
- ✓ Anaonyesha umuhimu wa mwanamke katika jamii
- ✓ Anaendeleza ploti
- ✓ Anaendeleza maudhui ya Ulevi
- ✓ Kupitia yeye tunapata sifa za Yona kuwa mwajibikaji
- ✓ Anatoa taswira ya wale wanaokubaliana na mabadiliko katika jamii
- ✓ Kupitia yeye tunapata sifa za sara kuwa mvumilivu
- ✓ Anaonyesha athari za watoto kulelewa na Yaya.

5a. **Mbinu za Kimtindo**

- ✓ Tashbihi - …kama safari ya ahera
- ✓ Tabaini – si pa mvua, si pa jua
- ✓ Tashihisi – Upepo kutupiga tukiwa hewani
- ✓ Istiara – mwendo ni wajibu
- ✓ Kinaya – Ata likachomeka haliwezi kufumiwa moto
- ✓ Taswira hisi – upepo kutupiga tukiwa hewani

b. **Usaliti katika Bembea ya maisha**

- ✓ Yona anamsaliti sara kwa kumpiga na kumsababishia ugonjwa wa moyo.
- ✓ Bunju na Neema wanamsaliti mwanao kwa kutompeleka 'out'
- ✓ Yona anasaliti utamaduni kwa kujipikia na kuteka maji kisimani Sara alipokuwa hospitalini.
- ✓ Viongozi wanasaliti wananchi kwa kutoleta maendeleo vijijini.
- ✓ Yona anasaliti hadhi yake kama msomi kwa kuingilia ulevi na kufutwa kazi.
- ✓ Yona anasaliti wanafunzi wake anapopokea ulevi kiasi cha kushindwa kwenda kazini.
- ✓ Yona anasaliti dini baada ya kuingilia ulevi Kwani alikua miongoni mwa watu wa kwanza kuingia kwenye dini.
- ✓ Yona anasaliti wanawe wa kike Kwani hakufurahia vile hakuwa na mrithi.
- ✓ Wafanyikazi wanawasaliti waajiri kwa kutoajibikia kazi.
- ✓ Vijana wanasaliti vijiji vyao Kwani wanaposoma hawataki kurudi kijijini mfano Asna
- ✓ Bunju anasaliti Neema kihisia. Anamkejeli kuwa alimpata hali mahututi.
- ✓ Wazazi wanawasaliti wanao kwa kukosa muda wa kutangamana nao mfano Neema na Bunju
- ✓ Bunju anamsaliti Neema kwa kutompea pesa za kugharamia matibabu ya mamake.
- ✓ Bunju anamsaliti Neema kwa kutomkubali mamake kulala kwake.
- ✓ Neema anasaliti utamaduni kwa kumtaka mamake alale kwake.

Teacher.co.ke

# SEHEMU D (USHAIRI)

## 7a

- ✓ Binadamu anakero
- ✓ Binadamu huwa hataki kunyang'anywa kilichochake
- ✓ Binadamu hudhulumu wenzake
- ✓ Binadamu hutwaa kile hajapewa
- ✓ Binadamu ni mbishi
- ✓ Binadamu ni mchokozi

**b.**

- ✓ Lina beti tano
- ✓ Mishororo minne katika kila ubeti
- ✓ Mizani kumi na sita katika kila mshororo
- ✓ Vipande viwili katika kila mshororo
- ✓ Vina vya ndani vinabadilika ilhali vya nje vinatiririka isipokuwa kiishio

c. Takriri – Kiumbe binadamu
Tashihisi- Adhabu zikamfike
Utohozi – Puresha

d. Inkinsari – Kilo chake (Kilicho chake)
Utohozi – Puresha
Kubadili msimbo – kama hayo kitendewa (Kitendewa kama hayo )
Tabdila- Ambae (ambaye)

e. Binadamu anatabia ya kutwaa asichopewa na kuwa mbishi. Ni kasoro yake kutokiri ikubalike akitendewa kama hayo.

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes



Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

# SEHEMU E ( FASIHI SIMULIZI)

8a i. Semi

ii .

a) Huwa fupi kwa kuwasilisha ujumbe mrefu kwa maneno machache.
b) Ni tanzu tegemezi kwa hutegemea tanzu nyingine kama vile hadithi, mazungumzo, n.k.
c) Hazibadiliki vivi hivi.
d) Baadhi ni kielelezo cha maadili k.v. methali.
e) Hutumia lugha ya kimafumbo.
f) Huibua taswira.
g) Huwa na mchezo wa maneno.
h) Baadhi huwa na muundo maalum k.v. methali na vitendawili.
i) Nyingine ikikosa kutumika hutoweka k.v. misimu.

b i .

- ✓ Huweza kudumu na kufikia vizazi vingi
- ✓ Huhifadhi toni na kiimbo
- ✓ Mkusanyaji aweza rudia uwasilishaji iwapo hakuelewa
- ✓ Kupata habari za kutegemewa na kuaminika
- ✓ Kupata hisia halisi za uwasilishaji.
- ✓ . Yaweza kutumika katika mazingira ambamo mmoja hawezi andika.

ii .

- ✓ Chaweza kukosa nguvu za umeme
- ✓ Hakiwezi kunasa uigizazi
- ✓ Ni ghali kununua vifaa vya kunasa sauti
- ✓ Fanani huenda asiwasilishe vyema akijua anarekodiwa.
- ✓ Kunaweza kuathirika na kelele za mazingira.
- ✓ Vinaweza kuchukua sauti zisizohitajika katika habar

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes